

# Kigamboni leo



Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni      June 2016- June 2020      Toleo Namba 01  
**JARIDA LA MIRADI YA MAENDELEO KIGAMBONI**

**Utekelezaji wa Miradi ya maendeleo iliyo-fanywa na Serikali ya awamu ya 5 Mwaka 2016 hadi 2020**



## **TAHARIRI**

**K**aribu mpenzi msomaji wa Jarida la Kigamboni leo, ambapo lengo la jarida hili ni kuonesha utekelezaji wa miradi mbalimbali katika sekta ya Afya, Elimu, Utawala, Maji na utoaji wa asilimia 10% kwa wanawake vijana na watu wenyewe ulemavu iliyolengwa na Serikali ya awamu ya 5 kwa kipindi cha mwaka 2016 hadi 2020 katika kuhakikisha wananchi wanasogezewa huduma karibu.

## **UTANGULIZI**

**H**almashauri ya Manispaa ya Kigamboni ni moja kati ya Manispaa 5 zinazounda Jiji la Dar es Salaam, ambapo upande wa kusini mwa jiji hilo inapakana na Manispaa ya Temeke, Wilaya ya Mkuranga na Bahari ya Hindi (fukwe yenye urefu wa kilomita 60).

Awali Kigamboni ilikua sehemu ya Manispaa ya Temeke mpaka mwaka 2015 ilipotangazwa rasmi kupitia gazeti la Serikali lenye GN No.462 kuwa Manispaa kamili inayojitegemea. Hata hivyo Kigamboni ilianza rasmi kutekeleza majukumu yake kama Manispaa mnamo Septemba 2016.

Kijiografia Kigamboni ina ukubwa wa Kilometra za mraba 577.9 sawa na Hekta 57.786.8 ambapo kiutawala Kigamboni ina Tarafa 3 yaani Kigamboni, Somangila na Pembamnazi , kata 9 na Mitaa 67. Pia inajumla ya madiani 15 kati yao wawili ni wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Idadi ya watu wa Kigamboni imeongezeka kutoka sensa ya mwaka 2012 iliyokuwa na jumla ya watu 162,932 ( wanawake 51.9% wanaume 49.1%) mpaka kufikia watu 225,938 ( wanaume 44.6% wanawake 55.4%) mwaka 2018. Idadi kubwa ya watu wa Kigamboni ni Vijana kuanzia miaka 20-34, pia wapo watoto wengi wenyewe umri chini ya miaka 5 ambapo idadi ya wazee wenyewe umri kuanzia 60 ni ndogo ukilinganisha na makundi mengine. Eneo kubwa la Kigamboni ni tambarare lenye muinuko kati ya 20m-50m, ina maeneo machache yaliyoinuka zaidi ya 100m-120m, ambapo eneo kubwa bado halijaendelezwa mbali na kuwa limekwishapimwa kwa asilimia 60.

Shughuli kuu za kiuchumi ambazo wananchi wake wanategema ni utalii, uvuvi, kilimo, ufugaji na biashara ndogondogo.

### **DIRA(VISION)**

*Kuwa na jamii ilioelimika na yenye maisha bora ifikapo 2022.*

### **DHAMIRA (MISSION)**

*Kutoa huduma bora za kijamii na kiuchumi kwa kutumia kiufasaha rasilimali zilizopo na utawala bora kwaajili ya kuboresha maisha ya wananchi.*

## **LINATOLEWA NA:**

Ofisi ya Mkurugenzi  
Halmashuri ya Manispaa ya Kigamboni  
S.L.P 36009  
Dar es Salaam  
Email: info@kigambonimc.go.tz **Tovuti:** [www.kigambonimc.go.tz](http://www.kigambonimc.go.tz)   Kigambonimanispaa

## Huduma za Afya Zilivyoboresha na kunufaisha wananchi Kigamboni

**H**almashauri ya Manispaa ya Kigamboni tangu kuanza utekeleazji wake wa majukumu kama Manispaa inayojitegema mwaka 2016 haikuwahi kuwa na Hospitali ya Wilaya wala vituo vyenye uwezo wa kutoa huduma nzuri za afya kwa wananchi wake hadi hapo Serikali ya awamu ya 5 ilipoamua kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini.

Kigamboni baada ya ukosefu wa Hospitali ya Wilaya kilichokua kituo cha afya cha Vijibweni Kilipandishwa hadhi na kutumika kama Hospitali ya Wilaya kwa wakazi wake na maeneo ya jirani ili kukidhi utoaji wa huduma za afya .

Kuanzia mwaka 2016/17 hadi Septemba 2019 Serikali ya awamu ya tano imetekeleza miradi ya afya yenye thamani ya Tsh. 4,620,745,086.68 Jumla ya Zahanati 3 zimejengwa na kukamilishwa kwa gharama ya Tsh. 265,616,680.20

Upanuzi wa vituo vya afya 2 vya Kigamboni na Kimbiji umefanyika kwa gharama ya Tsh. 914,429,385.00, Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kigamboni jumla ya Tsh. 1,500,000,000.00 zimepokelewa na majengo yote saba yamekamilika kwa awamu ya kwanza.

Ujenzi wa jengo la uchunguzi umekamilika na umegharimu Tsh. 101,938,725.00 Aidha, ununuzi wa vifaa tiba na vitendanishi kama X-rays mashine 2 na Ultra sound 1 zenye thamani ya Tsh. 386,000,000.00 umefanyika.

Mbali na uboreshaji wa miundombinu ya Afya, jumla ya Tsh. 458,892,000.00 zimepokelewa katika jitihada nzima ya uboreshaji wa huduma za afya kupitia fedha za Mfuko wa Pamoja (HSBF) na Tsh. 936,068,296.48 za ununuzi wa dawa, vifaa tiba na toka bohari kuu ya dawa MSD na Tsh. 57,800,000.00 za ununuzi wa dawa za viuatilifu kwa kipindi cha kuanzia 2016/2017 hadi 2018/2019.

### UBORESHWAJI WA KITUO CHA AFYA KIMBIJI



### Jengo la Mama na Mtoto Kituo cha Afya Kimbiji

Hadi kufikia Desemba 2017 Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ilikua mionganini mwa Halmashauri zilizobahatika kupokea fedha kutoka Serikali kuu chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa TAMISEMI Kiasi cha milioni 400 ikiwa ni mpango wa maboresho ya vituo vya afya kote nchini.

Kituo cha Afya Kimbiji kilianza uboreshaji wake kuanzia Februari 2018 ambapo kililenga kujenga majengo ya mama na mtoto, chumba cha upasuaji, maabara ya kisasa, na jengo la kuhifadhia maiti ambalo hapo awali halikuwepo.

Hadi kukamilika na kuanza kutoa huduma kwa kituo hiki kiasi cha shilingi milioni 514.4 zimetumika ambapo Serikali kuu ilitoa kiasi cha shilingi milioni 400 na Manispaa kuchangia kiasi cha Milioni 114.4 ili kuboresha zaidi huduma za Afya kwa wakazi wa Kimbiji na maeneo ya Jirani.

## Huduma za Afya Zilivyoboresha na kunufaisha wananchi Kigamboni



*Hadi kufikia  
juni jumla ya  
operation 60  
zimefanyika,  
25 za mama  
wajawazito na  
35 nyingine,  
operation zote  
zimefanikiwa  
kwa kiwango  
kikubwa.*

### *Chumba cha upasuaji kilicho jengwa kwenye kituo cha Afya Kimbiji*

Kituo hiki kimekamilika kwa asilimia 100 na huduma zote zinatolewa ambapo hadi kufikia Juni 2020 upasuaji 60 zimefanyika kwa ufanisi na mafanikio makubwa.

Aidha Watumishi wapatao 32 wa afya wenye fani mbalimbali wamepelekwa kwenye kituo hicho ili kuboresha utoaji wa huduma za afya zinazotolewa mahali hapo.



*Wodi ya mama na mtoto muonekano wake wa  
ndani katika kituo cha Afya kimbiji na kushoto ni  
muonekano wa jengo hilo kabla ya kuboreshwa kwa  
kujengwa majengo mapya.*

## Huduma za Afya Zilivyoboresha na kunufaisha wananchi Kigamboni

### UBORESHWAJI WA KITUO CHA AFYA KIGAMBONI

Tkiwa ni mwendelezo wa Serikali wa kuhakikisha huduma za afya zinaboresha kwa wananchi wote, Halmshauri ya Manispaa Kigamboni Julai 2018 ilipokea tena kiasi cha shilingi Milioni 400 kutoka Serikali kuu ili kuboresha kituo cha afya Kigamboni ambacho kabla ya upanuzi kilikua na changamoto ya kuzidiwa na wagonjwa hali iliyo-pelekea kudhoofu kwa utolewaji wa huduma.

Upanuzi wa kituo cha afya kigamboni umefanikisha kuongeza majengo ya mama na mtoto, jengo la kuhifadhia maiti ambalo halikuwe-po hapo awali, jengo la upasuaji na maabara ya kisasa yenye vifaa vyote ambapo hadi sasa ujenzi umekamiliaka na huduma zote zimeanza kutolewa.

Uboreshaji wa kituo hiki umeweze-sha wananchi kupata huduma zote za msingi hususani kupunguza vifo vya mama na mtoto, kuzidiwa kwa wagonjwa kulikokuwa kunasababishwa na ufinyu wa majengo ya kutolea huduma.



*Muonekano wa ndani ya jengo la Maabara ya kisasa yenye vifaa vyote muhimu iliyojengwa kwenye kituo cha Afya Kigamboni na tayari huduma zote za maabara zinapatikana*



*Jengo la wazazi na jengo la upasuaji (kushoto) yamejengwa kwenye kituo cha Afya Kigamboni*

## **Huduma za Afya Zilivyoboresha na kunufaisha wananchi Kigamboni**

### **UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA KIGAMBONI**



**Jengo la OPD likiwa limekamilika na tayari baadhi ya huduma zimeanza kutolewa.**

**K**atika Mpango wa Serikali wa kuhakikisha kila wilaya inakua na Hospitali yake, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ilitengewa Bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi huo ambaao umefanikisha kujengwa kwa Hospitali eneo la Gezaulole Kata ya Somangila lenye ukubwa wa ekari 38 mkabala na Ofisi za Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi.

Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya kwa hatua za awali umehusisha majengo 7 yaani jengo la utawala, jengo la mama na mtoto, maabara, jengo la kufulia , jengo la kuhifadhia dawa, jengo la wagonjwa wa nje (OPD), maabara na jengo la mionzi.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Dkt. Charles Mkombachepa amesema kuwa ukamilishwaji wa Hospitali hii utakua msaada mkubwa kwa wakazi wa Kigamboni na maeneo ya jirani kwani kwa sasa kuna huduma ambazo zinaposhindikana katika vituo vya afya na Hospitali ya Vijibweni inawalazimu wagonjwa kupelekwa Temeke au Muhimbili.

“ Mara tutakopokamilisha kabisa mradi huu wa hospitali huduma zote za msingi zitatolewa katika Hospitali yetu ya Wilaya na wananchi hawatasumbuka tena kufata huduma mbali na Kigamboni” alisema Mganga Mkuu.

### **UJENZI WA FORCE ACCOUNT**

Mfumo huu wa force account ambaao hutumia mafundi wadogo bila kufuata utaratibu wa kikandarasi

vyote vya Afya na Hospitali ya Wilaya ambapo Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni Arch. Ng'wilabuzu Ludigija amesema ni mfumo rahisi katika kutekeleza miradi kwa unafuu zaidi.

Mkurugenzi alisema kuwa ni dhana potofu kwamba kutumia mafundi wadogo ubora wa miradi hauzingatiwi kwani, Halmashauri wanao wataalamu wa ujenzi, wasanifu majengo na wakadiria majengo ambaao ndio wasimamizi wa miradi hiyo kuanzia hatua ya awali hadi ukamilishaji ili kuhakikisha kilichopangwa kinafanyika na kukamilika kwa viwango.

“ Mafundi tunaowatumia kwenye force account ndio hao wenye kampuni kubwa ambaao kama tungetumia mtindo wa ukandarasi wangetumika haohao kufanya kazi, tofauti ni kwamba ....



**Muonekano wa majengo na namna njia zinazojengwa zitakavyounganisha majengo yote ili kurahisisha utoaji huduma**

## Huduma za Afya Zilivyoboresha na kunufaisha wananchi Kigamboni

kwenye ukandarasi mkandarasi angekabidhiwa sehemu ya ujenzi wa mradi, angenunua vifaa ,angejenga na kukabidhi mradi ukiwa umekamilika mfumo ambao upo kisheria lakini ni gharama kubwa ukilinganisha na huu wa force account” alisema Mkurugenzi.

Mkurugenzi amesema kuwa anamshukuru Mhe.Rais na Uongozi wake kwa namna ulivyosaidia kusogea na kuboresha huduma za afya kwa wananchi wa Kigamboni ambao hapo awali walikuwa wakipata changamoto katika kuzifikia huduma kulingana na umbali wa maeneo wanayoishi.

### **MANUFAA YA UBORESHWAJI WA VITUO VYA AFYA NA UJENZI WA HOSPITALI**

Uboreshaji wa huduma za afya utapelekea kuwa na jamii yenyeye afya na hivyo kulinda nguvu kazi ya taifa, Kusogea huduma karibu na jamii kwakua hapo awali iliwalazimu kutembea umbali mrefu kufuata huduma, uwepo wa Hospitali ya Wilaya ambapo hapo awali haikuwepo kutasaidia Kupunguza vifo vya wanawake na watoto chini ya miaka 5.

Miradi hii pia itapunguza usumbufu na gharama za usafiri ambazo wananchi walikuwa wanatumia kwenda maeneo ya mbali kufuata huduma za Afya.



*Jengo la maabara likiwa limekamilika na katikati ni ujenzi wa njia itakayounganisha na majengo mengine.*



*Jengo la mama na mtoto likiwa limekamilika na mafundi wakiwa wanaendelea na ujenzi wa njia zinazounganisha na majengo mengine.*

## Tulipotoka na Tulipo kwa sasa Kiutawala



### Lililokuwa Jengo la ofisi za Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya Mjimwema

Tangu kuanza kwa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ofisi za Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya kwaajili ya kutolea huduma zilikuluwa za kukodi wakati utekelezaji wa ujenzi wa ofisi mpya eneo la Gezauole Kata ya Somangila ukiendelea.

Kuanzia mwaka 2016/17 hadi June 2020 Serikali ya awamu ya tano imetekeleza miradi ya Kiutawala ndani ya Manispaa yenye thamani ya

Tsh. 5,460,000,000.00 ambapo mpaka sasa jumla ya Tsh. 4,300,000,000.00 zimepokelewa toka Serikali kuu ili kuiwezesha Manispaa kuwa na ofisi tulivu na bora ya utoaji wa huduma kwa wananchi.

Ujenzi wa jengo la Utawala la Mkurugenzi ulianza tarehe 27/1/2018 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 26/9/2018 lakini kutokana na changamoto za mvua haikuwezekana kukamilika kwa wakati hivyo kupelekea Mkandarasi kuongezewa muda ambapo Kwa sasa Ofisi zimeshaanza kutumika wakati hatua za ukamilishaji zikiendelea .

Hata hivyo Halmashauri imeanza pia ujenzi wa nyumba ya makazi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni, hadi sasa ujenzi upo hatua za awali za utekelezaji na Jumla ya Tsh. 60,000,000.00 toka mapato ya ndani zimetolewa kwa utekelezaji huo.



*Jengo jipywa la utawala la Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni lililojengwa eneo la Gezauole Kata ya Somangila na kushoto ni ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi.*

## Tulipotoka na Tulipo kwa sasa Kiutawala

Kwa upande mwingine wa Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni linatarajiwa kugharimu kiasi cha Tsh. 1,618,149,133 .00 hadi kukamilika kwake , jumla ya Tsh. 1,100,000,000.00 zimepokelewa toka Serikali Kuu na kutumika katika ujenzi jengo hilo. Ujenzi upo hatua za ukamilishaji na limeanza kutumika.

Viongozi wa Kigamboni wanashukuru kupata miradi hii ya kiutawala inayowawezesha kufanya kazi kwenye mazingira mazuri kwani Kukamilika kwa Ofisi hizi kwa kiwango cha kuweza kuhamia kumeweza kuokoa fedha za kodi zilizokuwa zikilipwa awali kwenye jengo la kukodi lililokuwa Mjimwema kiasi cha Tsh. 2,600, 000 kwa mwezi ambapo kwa mwaka ilikuwa Tsh. 31,2000,000.

Ikumbukwe kuwa Ofisi za Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni zilihamza rasmi kutoka kwenye ofisi za Mjimwema kwenda Kata ya Somangila, Gezaulole mnamo tarehe 30 Agust 2019.



*Jengo la ofisi za Mkuu wa Wilaya Kigamboni lililojengwa eneo la Gezaulole Kata ya Somangila.*

*Kwa ujumla majengo haya ya utawala yamewezesha Viongozi na watumishi kufanya kazi katika mazingira mazuri sana.*

**Bilioni 1.4 asilimia 10 ya mapato ya ndani yanufaisha vikundi 466 vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu kwa kipindi cha mwaka 2016-2020.**

**K**atika kuboresha hali za kiuchumi za wananchi msisitizo wa Serikali ya awamu ya 5 ulikua ni kuhakikisha kila Halmashauri inatenga asilimia 10 kwaajili ya mikopo ya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni imefanikiwa kutenga na kutoa Jumla ya Bilioni 1.4 kwa vikundi 466 Tangu kuanzishwa kwa Manispaa hii kuanzia mwaka 2016 hadi 2020.



*Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Sara Msafiri akitoa hundi ya fedha ya mikopo kwa mmojawapo ya kikundi cha watu wenye ulemavu kipindi cha kufunga mwaka wa fedha 2018/2019 Mjimwema.*

## KIGAMBONI LEO

**Bilioni 1.4 asilimia 10 ya mapato ya ndani yanufaisha vikundi 466 vya Wanawake, Vijana na Watu wenyewe ulemavu kwa kipindi cha mwaka 2016-2020.**

Kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17 jumla ya vikundi vya vijana 12 na Wanawake 23 vimepatiwa mikopo yenyne thamani ya Tsh. 88,950,600, Kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18 jumla ya vikundi vya vijana 76 na Wanawake 19 vimepatiwa mikopo yenyne thamani ya Tsh. 231,394,000 na Kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 kiasi cha Milioni 500 zimetolewa kwa vikundi vya wanawake 92, walemauvu 08 na 54 Vijana na 2019/2020 kiasi cha Tsh. milioni 616 kimetolewa kwa vikundi 182 Wanawake 126, Vijana 51 na Walemauvu 5 hivyo kufanya jumla ya Bilion 1.4 kutumika kuweshesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenyewe ulemavu .

Lengo kuu la Serikali kuhimiza utowaji wa mikopo hii ni kuwawezesha wananchi kupata mikopo isiyokuwa na riba,

**Utoaji wa vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo wadogo na vitambulisho vya matibabu kwa wazee**

**K**atika kutekeleza agizo la Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. John Joseph Magufuli, Wilaya ya Kigamboni imefanikiwa kutoa vitambulisho vya wajasiriamali 22,000.

Aidha Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Sara Msafiri amekipa thamani kitambulisho hicho kwa kuungana na uongozi wa CRDB Benki baada ya kukubali ombi lake la kuwawezesha wajasiliamali walio na vitambulisho vya ujasiliamali kwa kusaini mkataba utaowawezesha kutumia vitambulisho vyao kuwa dhamana ya kupata mikopo ili kuinua uchumi wao.

Kutambua makundi maalumu hasa watu wenyewe ulemavu, wanawake na vijana kuwawezesha kujikwamua kiuchumi, Kuongeza idadi ya wajasiriamali katika Wilaya na mzunguko wa fedha kwenye uchumi pamoja na Kuongeza ustawi wa jamii .



*Mbunge wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Faustine Ndungulile alipotembelea kuona bidhaa zinazozalishwa na wanawake kwenye hafla ya kuweshesha wanawake kiuchumi iliyofanyika Mjmwema Jan 2018.*



*Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Sara Msafiri akimkabidhi mmoja wa wajasiliamali wadogowadogo kitambulisho cha ujasiliamali eneo la Feri katika hafla ya utoaji wa vitambulisho iliyofanyika hapo*

## Utekelezaji wa agizo la Utoaji wa Vitambulisho vya matibabu bure kwa wazee

Manispaa ya Kigamboni ina jumla ya wazee wapatao 4893, mpaka sasa Manispaa ya Kigamboni imefankiwa kutoa vitambulisho kwa wazee 3518 ambayo ni sawa na asilimia 72 ya wazee wote.

Lengo la Serikali la kuhakikisha kila Halmashuari inatoa vitambulisho vya matibabu kwa wazee ni kuwarahisishia wazee kupata matibabu kwa haraka (kupewa kipaumbele) ambapo pia itasaidia Halmashauri kupanga na kutoa huduma kwa wanufaika kwa urahisi hatimaye wazee watapata matibabu bure



*Mkuu wa Wilaya Mhe.Sara Msafiri akikabidhi kitambulisho cha matibabu bure kwa mmoja wa wazee waliofika kwenye uzinduzi wa utoaji vitambulisho Mjmwema.*

## Miradi yenyeye thamani ya Bilioni 1.8 imetekelizwa kwenye idara ya Elimu Msingi kuanzia Mwaka 2016 hadi 2020

Kuanzia mwaka 2016/17 hadi June 2020 Serikali ya awamu ya tano imetekeliza miradi ya Elimu msingi yenyeye thamani ya Tsh. 1,803,896,414.48. Jumla ya madarasa 56 yamejengwa kwa gharama ya Tsh. 554,500,001.

Aidha ukarabati wa madarasa 17 umefanyika kwa gharama ya Tsh. 47,090,101.56 na matundu ya vyoo 125 yamejengwa kwa gharama ya Tsh. 423,261,700.00 pia shule mpya 3 (Kigogo, Mwanzomgumu, na Mikenge) zimejengwa kwa nguvu ya wananchi na Serikali imechangia Tsh. 82,000,000.

Kwa upande wa Madawati, Jumla ya madawati 3,470 yenyeye thamani ya Tsh. 416,400,000.00 yalipokelewa toka Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kama mgao kwa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni.

Aidha madawati 750 yenyeye thamani

ya Tsh.74,094,000elfu yemeweza kutengenezwa na Manispaa.

Maispaa ya kigamboni imejenga nyumba za walimu 2 (S/M Kijaka 1 na Vumiliaukooni 1) kwa gharama ya Tsh. 132,758,861.48 fedha toka mapato ya ndani (OS) ili kuboresha mazingira bora ya walimu katika kukuza Taaluma za Wanafunzi.

Kutokana na uboreshwaji wa miundombinu ya elimu na mpango wa elimu bure umepelekeea ongezeko la wanafunzi wanaoandikishwa darasa la kwanza, kutoka 5541 kwa mwaka 2017 ikiwa ni 98% ya idadi ya wanafunzi 5628 iliyotarajiwa hadi 6071 kwa mwaka 2019 ikiwa ni 108% ya idadi ya wanafunzi 5618 iliyotarajiwa



*Majengo ya vyumba vya madarasa 2 (mawili) Vijibweni Shule ya Msingi yaliyojengwa kwa fedha za EP4R Lipa kulingana na matokeo*

## KIGAMBONI LEO

**Bilion 2.9 Zimetumika kuboresha miundombinu ya Elimu Sekondari kwa mwaka 2016 hadi 2020.**



**Shule ya Sekondari Paul Makonda iliyopo kata ya Kigamboni ikiwa imekamilika na kuruhusu wanafunzi wa kidato cha kwanza kuingia mwaka 2020.**

Kuanzia mwaka 2016/17 hadi June 2020 Serikali ya awamu ya tano imetekeleza miradi ya Elimu ya sekondari yenyeye thamani ya Tsh. 2,993,491,061.29

Jumla ya madarasa 22 yamejengwa na madarasa 71 kukarabatiwa kwa gharama ya Tsh.526,869,392.59 na Tsh.26,552,327.00 zimetumikakatika ukarabati wa maabara ya shule ya Sekondari Aboud Jumbe na milioni 18 ukarabati wa maabrara ya Nguva Sekondari.

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni pia ilipokea Tsh. 262,500,000.00 toka Serikali kuu kama ruzuku maalumu ya ukamilishaji wa miradi viporo (Maboma) ambapo miradi kadhaa imekamilika na mingine ipo hatua za ukamilishaji.

Aidha, Ujenzi wa mabwalo ya chakula 3 kwa gharama ya Tsh. 310,000,000.00 yamejengwa katika shule za Sekondari za Nguva, Kisarawe II na Pembamnazi.

Ili kuhakikisha elimu bora inatolewa, jumla ya mabweni 4 yamejengwa katika Shule za Nguva (2) na Kisarawe II (2) kwa gharama ya Tsh. 554,444,744.70 na Ununuzi wa vitanda 160 kwa gharama ya Tsh. 28,000,000.00

Majengo 3 ya utawala yamejengwa chini ya uongozi wa Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na majengo hayo yapo hatua za ukamilishaji ambapo Serikali kuu ilichangia Tsh. 75,000,000.00



**Baadhi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza na waalimu wa Shule ya Sekondari Paul Makonda wakiwa kwenye picha ya pamoja**

## Bilioni 2.9 Zimetumika kuboresha miundombinu ya Elimu Sekondari kwa mwaka 2016 hadi 2020.

Ujenzi wa nyumba 2 za walimu (6 kwa 1) umefanyika kwenye shule mbili yaani Shule ya Sekondari Pembamnazi na Somangila kwa gharama ya Tsh. 448,315,060.00 fedha za SEDEP ambapo ujenzi umekamilika na nyumba zinatumika .

Kwaupande wa ununuzi wa madawati 1403 umefanyika kwa gharama ya Tsh. 229,562,000.00 na ujenzi wa matundu ya vyoo 141 yenyе thamani ya Milion377.3 , ukarabati wa chumba cha kompyuta shule ya Sekondari Kimbiji kwa thamani ya Tsh.14,273,030.41 pia ukarabati wa maabara Nguva Sekondari uliogharimu Mil.18.

Aidha shule mpya ya Sekondari ya Paul Makonda iliyopo Kata ya Kigamboni imejengwa kwa gharama ya Tsh. 309,852,638.00 na tayari imekamilika na kutumika kwani imechukua wanafunzi 98 wa kidato cha kwanza Januari 2020 .

### FAIDA ZA UBORESHWAJI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU

Kukamilika kwa miundombinu ya shule imesaidia kuboresha mazingira mazuri kwa wanafunzi ya kujifunzia na walimu kufundishia hali itakayopelekea Kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.


Ujenzi wa Sekondari mpya ya Paul Makonda iliyopo Kata ya Kigamboni umesaidia watnafunzi kupata Shule karibu na makazi yao pia kuiweshesha Kata ya Kigamboni kupata Shule ya Sekondari ya Serikali kwani ni Kata pekee katika wilaya nzima ya Kigamboini ambayo haikuwa na Shule ya Kata ya Sekondari.



*Moja ya Bweni la wanafunzi wa Kiume wa Kidato cha Tano Shule ya Sekondari Nguva*

Elimu Bure imesaidia Kuongeza idadi ya usajili wa wanafunzi wa darasa la kwanza na kidato cha kwanza.

Ujenzi wa Mabweni na madarasa, Maktaba katika Shule ya Sekondari Nguva , Kisarawe II NA Abdujumbe imesaidia kuwa na shule ya upili(Kidato cha tano na sita) kwa kuwa hapo awali Wilaya haikuwa na Shule za kidato cha tano na sita



*Muonekano wa ndani ya Bweni la wanafunzi wa kiume kwenye Shule ya Sekondari Nguva yenyе kidato cha tano na sita kwa Hamlashauri nzima ya Kigamboni.*

## KIGAMBONI LEO

### Mradi Mkakati wa Ujenzi wa Soko la Kisasa Kibada.

Katika kuhakikisha Halmashauri zote nchini zinajitengenezea mazingira ya kujitegemea kifedha kupitia fursa za masoko ya mitaji na uwekezaji, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ni mionganoni mwa Halmashauri iliyofanikiwa kupata mradi mkakati mmoja wa Ujenzi wa Soko la Kisasa la Kibada linalojengwa kwenye Kata ya Kibada.

Mradi huu upo kwenye hatua za awali na utagharimu kiasi cha Tsh.6.6 Bilioni hadi kukamilika,Jengo hili la kisasa litajengwa na Mkandarasi Mwananchi Engineering and Construction Company Ltd (MECCO) huku Mhandisi Mshauri akiwa ni Bureau for Industrial Cooperation (BICO).

Ujenzi umeanza tarehe 16/08/2019 na unatarajiwa kukamilika 29/11/2020 ambapo hadi kukamilika kwa mradi mbali na kuongeza pato la Manispaa kwa kukusanya Kodi lakini pia utawezesha;  
Mradi wa soko utakapokamilika utapunguza adha ya umbali na gharama ya usafiri kwa wananchi waliokuwa wakifuata huduma za bidhaa za soko nje ya Wilaya, Wafanyabiashara zaidi ya 320 watanufaika na mradi huu kwa kuboreshewa mazingira mazuri ya kufanya biashara,  
Bidhaa za sokoni kama vile matunda mbogamboga zitashuka kwa kuwa zitakuwa zikipatikana karibu na kwa urahisi .



*Muonekano wa Soko la Kisasa Kibada baada ya kukamilika kujengwa.*



*Ujenzi wa Soko la Kisasa Kibada ukiwa kwenye hatua za awali (msingi)*

## **UJUE UTARATIBU WA KUPATA KIBALI CHA UJENZI MANISPAA YA KIGAMBONI**

### **1.KIBALI CHA UJENZI**

Kulingana na sheria ya uendelezaji miji ya mwaka 2004, na kanuni zake za mwaka 2008, si ruhusa kwa mtu yeyote kujenga au kuanza ujenzi wa aina yo yote bila:-

- (i) Kutuma maombi kwa mamlaka ya mji
- (ii) Kuwasilisha michoro ya jengo na kumbukumbu husika
- (iii) Kupata kibali cha maadishi kinachoitwa “Kibali cha Ujenzi”

### **2.KIBALI CHA AWALI (Planning Consent)**

Inashauriwa kupata kibali cha awali kabla ya kuomba kibali cha ujenzi.

Hivyo muendelezaji anatakiwa aandae michoro ya awali (outline plan) kwa utaratibu unaotakiwa ukionesha aina ya ujenzi anaokusudia kuufanya ili aweze kupata ridhaa ya kuendelea na hatua ya kuandaa michoro ya mwisho.

Katika hatua hii mambo yafuatayo yataangaliwa/yatakaguliwa:-

viwango vya ki-mipango na kisanifu (Planning and design spacestandards), ujazo wa jengo kwenye ardhi (Density of the building on land), urefu wa jengo/ idadi ya sakafu (height/number of floors), usanifu (Design)pamoja na sura na mkao wa jengo (Appearance and siting of building)

### **FAIDA**

\*Kuokoa muda na gharama iwapo michoro ya mwisho itaonekana kuwa na dosari za kitaalamu ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho.

\*Kuwa na uhakika kuhusu mahitaji muhimu ya kuzingatiwa wakati michoro inaandaliwa.

### **3.JINSI YA KUWASILISHA MAOMBI YA KIBALI CHA UJENZI.**

Baada ya michoro kukamilika, iwasilishwe ikiwa kwenye majalada kwa namna ambayo inaweza kufunguliwa na kusomeka. Michoro hiyo iwasilishwe kwa utaratibu ufuataao:-

Seti mbili za michoro ya kiusanifu (architectural drawings)

Seti mbili za michoro ya kihandisi (structural drawings) kwa majengo ya ghorofa ikiwa imeambatanishwa.

### **4.MICHORO ILIYOANDALIWA IONESHE NINI?**

Michoro itakayoandaliwa inatakiwa ioneshe mambo yafuatayo:-

- Namna jengo litakavyokuwa (plan, section, elevations, foundation and roof plan)

- Namba na eneo kiwanja kilipo

- Jina la mmiliki ardhi anayehusika

- Jina la mchoraji, ujuzi na anuani

- Ukubwa wa jengo au ujenzi wa aina yo yote kwa mita za mraba au kwa mita za urefu.

- Ujazo wa kiwanja (plot ratio)

- Matumizi yanayokusudiwa

- Umbali wa jengo kutoka kwenye mipaka ya kiwanja (setbacks).

- Mfumo wa maji taka

- Idadi ya maegesho yatakayokuwepo

### **5.VIAMBATISHO**

- Fomu za maombi zilizojazwa kwa usahihi

- Uthibitisho wa umiliki wa kiwanja (hati au barua ya toleo kwa viwanja vilivyopimwa, na hati ya mauziano kwa maeneo/viwanja ambavyo havijapimwa) pamoja na fomu ya utambuzi kutoka ofisi ya Mtendaji Kata/Mtaa.

- Mabadiliko ya matumizi ya ardhi kama mwombaji amebadili matumizi ya ardhi.

- Uthibitisho wa malipo ya kodi ya ardhi (kwa viwanja vilivyopimwa) kwa mwaka wa fedha unaoendelea.

### **6.UHAKIKI WA MAOMBI YA KIBALI**

- Uhakiki wa miliki

- Uchunguzi wa matumizi ya eneo/kiwanja (makazi, biashara, viwanda, taasisi, shule, n.k)

- Ukaguzi wa kiwanja kinachokusudiwa kuendelezwa

- Ukaguzi wa usanifu wa michoro

- Uchunguzi wa matumizi ya jengo

- Uchunguzi wa uwiano wa jengo

- Uchunguzi wa uimara na uwezo wa jengo

- Uchunguzi wa maofisa wa afya (mfumo wa maji taka, mzunguko wa hewa ndani ya nyumba, n.k)

- Uchunguzi wa tahadhari za moto

- Uchunguzi wa uzingatiaji wa mpango wa jumla wa uendelezaji (master plan/redevelopment plan) ulioidhinishwa

- Kuandaa orodha ya vibali vilivyokidhi vigezo.

- Kuwasilisha kwa Mkurugenzi wa Manispaa orodha ya vibali vilivyokidhi vigezo kwa ajili ya idhini

- Hatimaye kuandaa na kutoa kibali cha ujenzi.

## KIGAMBONI LEO

### Habari katika Picha



*Naibu Waziri TAMISEMI Mhe.Josephat Kakunda mwenye suti ya blu akipongeza uongozi wa wilaya ya kigamboni kwa kusimamia ujenzi wa soko la kisasa Kibada*

*Waziri wa TAMISEMI Mhe.Selemani Jafo akizungumza na mgonjwa aliyekuja kupata matibabu kwenye Hospitali ya Wilaya alipofanya ziara ya kuona huduma zitolewazo.*



*Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. John Pombe Magufuli akikata utepe ishara ya ufunguzi wa Wilaya ya Kigamboni uliofanyika februari 2020.*

*Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda akikabidhi vifaa magodoro kwaajili ya vitanda vya wagonjwa baada ya hafla ya kukabidhi vifaa vitakavyowezesha Hospitali ya Wilaya kuanza kufanya kazi.*